


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe

*James Mwangi[1*], Prof. Nabea Wendo, PhD[1] na Dkt. Sheila Wandera, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S. L. P. 1100 – 20300 Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: jamwamu09@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1252**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*15 Juni 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ushawishi, Mikakati, Mantiki, Hisia Na Imani, Tarakilishi, Kiupatanishi Facebook Na Baruapepe.*

**IKISIRI**

Mawasiliano yameimarika sana katika karne ya ishirini na moja kufuatia uvumbuzi wa teknolojia ya mawasiliano. Namna uvumbuzi unavyoendelea kuwepo ndivyo visa vya uhalifu wa mitandaoni vinavyozidi kuongezeka. Wahalifu hutumia baruapepe, Instagram, Twitter, WhatsApp, Facebook na njia nyinginezo za mitandaoni kuwadanganya watu, kuwaibia watu hela, kusambaza jumbe chafu za kiponografia, kuingilia data za wenyewe bila ruhusa na kusambaza jumbe za vitisho kwa watumiaji wa mitandao hii. Wahalifu hutumia ushawishi kutuma jumbe kama vile za ushindi wa pesa, ugawaji urithi, masuala ya kibiashara, jumbe za uhusiano wa kimapenzi na udukuzi wa pesa katika benki huku lengo kuu likiwa kuwaibia watu hela. Utafiti huu ulilenga kuchanganua mikakati ya ushawishi inayotumiwa na wahalifu hawa wa mitandaoni ili kufaulisha uovu wao. Nadharia ya Ubalagha ya Ushawishi iliyoasisiwa na Aristotle kisha kuendelezwa na wasomi wengine ilitumiwa pamoja na nadharia ya Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi iliyoasisiwa na Herring (2001). Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kimakusudi. Data ya utafiti ilikusanywa katika mitandao ya kijamii kwa njia ya upakuaji halafu kuhifadhiwa katika maandishi kisha ufafanuzi wake ulifanywa kwa njia ya maelezo. Mbinu ya uhakiki matini ilitumiwa katika uchanganuzi wa data. Utafiti huu ulibainisha kuwa wahalifu wa mitandao ya kijamii hutumia mikakati ya imani na dini, hisia, utoaji wa hoja zenye mantiki ili kuwashawishi watumiaji wa mitandao. Utafiti huu ni wa manufaa kwa watafiti wa lugha hasa katika nyanja ya Isimu kwa kuwapa ari ya kuchambua diskosi na kauli tofauti tofauti kama zinavyotumiwa katika mitandao ya kijamii.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1252

**APA CITATION**

Mwangi, J., Wendo, N. & Wandera, S. (2023). Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 180-193. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1252.

**CHICAGO CITATION**

Mwangi, James, Nabea Wendo and Sheila Wandera. 2023. "Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 180-193. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1252.

**HARVARD CITATION**

Mwangi, J., Wendo, N. & Wandera, S. (2023) "Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 180-193. doi: 10.37284/jammk.6.1.1252.

**IEEE CITATION**

J. Mwangi, N. Wendo & S. Wandera, "Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 180-193, Jun. 2023.

**MLA CITATION**

Mwangi, James, Nabea Wendo & Sheila Wandera. "Mikakati ya Ushawishi katika Jumbe za Kihalifu kwenye Facebook na Baruapepe". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jun. 2023, pp. 180-193, doi:10.37284/jammk.6.1.1252.

## UTANGULIZI

Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia kuongezeka na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano, jambo ambalo limebadilisha maisha ya watu wengi kama vile utendakazi wao, utafutaji wa elimu, mapenzi, utangamano na uhusiano (Ling & Baron, 2007). Hatua hii ya ukuaji wa teknolojia imechangiwa mno na intaneti, mitandao ya kijamii, simutamba na tarakilishi. Haya vilevile yamechangia pakubwa katika uhalifu kwenye mitandao ya kijamii. Man na Sutton (1998) wanadai kuwa mtandao huu wa kimawasiliano (intaneti) umejenga jukwaa kubwa na nafasi ya wahalifu kulaghai kundi kubwa la watumiaji na kusababisha madhila kwenye vyombo vya usalama na vya kutekeleza sheria. Facebook na baruapepe ni mitandao miwili ya kijamii ambayo huruhusu watu kutagusana na kushirikiana kwa kutumia lugha watakayo na kwa njia waipendayo. Ushirikiano huu kwenye intaneti husaidia katika biashara za mitandaoni, kujenga urafiki, kuchumbiana, na shughuli za masomo.

Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi huwapa watu uhuru wa kuandika, kutuma jumbe, picha na video bila kuwa na woga wowote wa kufuatwa na mtu (Crystal, 2011). Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi ni mawasiliano kwa njia ya tarakilishi zilizounganishwa kwa kutumia intaneti na waliounganishwa hushirikiana kwa kuwasiliana na watu wa ulimwengu mzima (De La Fuente, 2003). Herring (2004) anasema kuwa mawasiliano haya huhusisha arafa au jumbe na wahusika hushirikiana mmoja kwa mwingine kwa kupiga chapa ujumbe kwenye tarakilishi na husomwa na wengine kwenye skrini zao mara moja au baada ya muda fulani. Uhuru huu wa watu kuandika wanachokitaka katika mitandao ya kijamii umesababisha mlipuko wa uhalifu (Hayward & Yar, 2006). Montague (2011) anadai kuwa uhalifu huu wa kulaghaiwa umerahisishwa kwa kuwa mtu hahitajiki kusafiri katika sehemu moja ili atekeleze wizi. Zaidi ni kuwa uhalifu huu huwa wazi kwa sababu hufahamu mtu unayeshirikiana au kufanya biashara naye.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Fadhilah (2010) alichunguza mikakati ya ushawishi inayotumiwa na watangazaji wa bidhaa katika runinga. Utafiti huu ulionyesha kuwa mtangazaji katika matangazo ya kibiashara ya DRTV alitumia mikakati mingi ya ushawishi huku akiongozwa na nadharia ya Gorys Keraf kuwashawishi watazamaji wake. Mikakati ya ushawishi iliyotumiwa ni kama vile; urazini, utambulisho, upendekezaji, makubaliano, utoaji wa fidia na uhamishaji. Mbinu hizi za ushawishi ziliwasilishwa kwa kutoa ithibati ya bidhaa zinavyofanya kazi na kuonyesha uhalali na uzuri wake halafu baadaye kuibua athari chanya ya mawazo kwa wateja wake. Mtangazaji alitumia kila aina ya mbinu kuonyesha wateja wake kuwa bidhaa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

zingine hazifai kutumiwa ila zake. Utafiti wake uliufaa utafiti huu pakubwa kwa kuwa, ameshughulikia mbinu zinazotumiwa kuwashawishi watu, sawa na utafiti huu.

Lea na wenzake (2009) walifafanua kwa kina mikakati ya ushawishi wakielezea kuhusu Saikolojia inavyohusiana na uhalifu. Walielezea kuwa watu kujipata katika mitego ya kulaghaiwa ni kwa ajili ya kufanya maamuzi na wahalifu kujenga hali fulani pamoja na uhalifu wao, ambao huongeza uwezekano wa kufanya uamuzi. Wanaamini kuwa aina mbalimbali za uhalifu katika jumbe na mitindo ya ushawishi huvutia zaidi. Walidhihirisha kuwa utambuzi (kujiamini sana katika mada fulani) na motisha hufafanua sababu za kisaikolojia zinazowafanya watu kujibu jumbe za kihalifu. Utafiti wa awali ulimfaa mtafiti kimawazo kwa kuonyesha sababu za watu kujibu jumbe za wahalifu.

Rusch na wenzake (1999) walidai kuwa wahalifu hutumia mikakati ya ushawishi ya kiwango cha juu zaidi katika uuzaji kuwaibia watu. Uchunguzi huu ulionyesha ufundi wa kiwango cha juu cha ushawishi kutoka kwa wahalifu kama vile, kutoa ahadi ambayo ni ya muda fulani au wanaweka makataa ya kupata zawadi ile. Hali hii huwafanya watu kufanya uamuzi kwa njia ya kuwaza kwa muda mfupi sana. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa mtafiti kwa sababu aliangazia ufundi zaidi unaotumiwa katika jumbe za mitandaoni kuwashawishi watumiaji.

Nabea (n.d) alichunguza vipengele muhimu katika jumbe za baruapepe pamoja na mikakati ya ushawishi inayotumiwa na wahalifu katika jumbe za baruapepe. Uchunguzi wake ulionyesha kuwa vipengele muhimu vinavyotawala jumbe hizi ni kama vile; muundo, utangulizi, maelekezo, vitendo tatanishi, utathmini na hitimisho. Matokeo yake yalionyesha kuwa ushawishi wa wahalifu hawa katika baruapepe hutokana na masuala ya kijamii pamoja na kiuchumi. Kazi ya mtafiti ilitumia msingi wa nadharia ya Majadiliano ila utafiti wa sasa ulijikita katika nadharia ya Ubalagha ya Ushawishi na nadharia ya Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi. Kazi yake ilifaa mno utafiti huu kimawazo na kinadharia.

Naksawat (2016) anadokeza vipengele saba vya ushawishi kama vilivyotambuliwa na (Dyrud, 2005) na Manson (2011) ambazo hufanya uhalifu wa mitandaoni kufaulu. Vipengele hivyo ni pamoja na: kubinafsisha uhalifu, kuchochea hamu angavu ya kupata hela, imani, kuwauliza walengwa kuchukua hatua chache na kuzifuata, kujenga uhalali na uaminifu na kuweka makataa bandia.

## MISINGI YA NADHARIA

Nadharia ya Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi iliyoasisiwa na Herring (2004) ilitumika katika utafiti huu. Kulingana na Ling (2014), nadharia hii huchunguza lugha na matumizi yake pamoja na uchanganuzi wa diskosi katika isimu katika mazungumzo ya mitandaoni kwa kuangazia mitindo na maana. Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi kama ilivyoelezwa ni mchakato ambao watu hutuma, hupokea, na kuelewa ujumbe uliotumwa kwa njia ya teknolojia kama vile; vyombo vya mawasiliano vilivyounganishwa kwa mtandao na huwezesha kuandika habari, kutuma habari na kuifasiri. Ufafanuzi huu umepata mabadiliko mengi kuanzia tu ile siku mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi yalipobuniwa. Nadharia hii ni muhimu katika kuchunguza jumbe za kihalifu kwenye Facebook na baruapepe kwa kuonyesha tabia za watumaji wa jumbe hizi (wahalifu) na namna zinavyofasiriwa na wapokeaji. Nadharia ya Ubalagha ya Ushawishi nayo iliasisiwa na Aristotle kati ya (384 KK -322 KK) kisha kuendelezwa na wanafalsafa wengine walioathirika na kazi yake kama vile; Burke (1950), Harold Barret (1974), Edwin Black (2007), Cicelo na Quintilian, Rapp (2010 ) na Perloff (2010). Aristotle aliibuka na mikakati mitatu ya ushawishi katika kazi ya Ubalagha ya Ushawishi (Perloff, 2010). Nadharia hii ilichunguza mikakati ya ushawishi katika jumbe za kihalifu kwenye mitandao hii miwili. Mikakati hii ni tofauti na hukusudia kushawishi hadhira kwa njia tofauti. Mikakati hii ni pamoja na: Mkakati wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

kiimani, mkakati wa pili ni wa kihisia na mkakati wa mwisho ni wa mantiki. Nadharia hizi mbili zilitumiwa kuonyesha sababu za kuwepo na kuendelea kwa uhalifu katika mitandao ya kijamii. Nadharia hizi zilidhihirisha kuwa wahalifu huwasilisha sifa zao nzuri huku wakitumia mbinu zote katika mitandao kuficha uovu na udhaifu wao kwa kuhusisha mikakati ya ushawishi na maneno yenye mvuto kugusa hisia za walengwa.


## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika kwenye mitandao ya kijamii (Facebook na baruapepe) huku mtafiti akipakua jumbe zilizooana na malengo ya kazi yake. Mtafiti pia alipekuapekua vitabu, tasnifu na majarida yaliyokuwa ya manufaa kwa kazi yake. Muundo wa utafiti huu ulijikita katika mkabala wa maelezo kwa kufafanua yaliyofungamana na uhakiki na uchambuzi wa yaliyopatikana kwenye jumbe hizi. Utafiti huu ulilenga jumbe za kihalifu katika mitandao hii miwili pekee bila kuzingatia wakati zilipoandikwa. Mitandao hii iliteuliwa kwa sababu inatumiwa sana na watu katika mawasiliano hivyo wahalifu wanatumia nafasi hii kuendeleza uhalifu wao. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ya kimakusudi na iliongozwa na madhumuni ya mtafiti. Mtafiti alikusanya jumbe kumi kisha kuzichuja hadi nne huku akiongozwa na malengo na maswali ya utafiti. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uhakiki matini.

## MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA

*Ujumbe A1* ni wa kimapenzi unaoandamana na picha ya mwanamume mtanashati, ukinuiwa kumshawishi msomaji kwenye mtandao.

**Ujumbe A1**




*Naam mpenzi, mimi ni Jenerali Mike Wilson. Mimi nimekuwa katika idara ya Uanajeshi kwa miaka thelathini…nimekuwa katika nchi ya Iraq kwa miaka minne na nina mipango ya kujiuzulu ili nikutane na mtu nimpendaye. Sijalishwi na umbali au miaka kwa kuwa najua umbali ni njia na umri ni nambari tu. Yote yahusiana na mtu atakayekufanya ufurahie na kukusadiki na kufanyia kama malkia. Mimi ndiye mvulana wa pekee wa marehemu wazazi wangu. Mimi ni mjane iliye na mtoto mmoja aitwaye Jeffery Wilson na nampenda sana…ana umri wa miaka 14.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*(https://www.facebook.com/100024187031900/posts/pfbid07u6XP76krHXrp1NFCYbBQ2Z1WKyxmiLWepJK2FJNrqTV85s581Afwqm5xJSUSrkQl/?mibextid=Nif5oz)*

*Napendezwa na:*

*Mimi nina umri wa miaka 54 na ninajitegemea kifedha. Napenda marafiki Na familia, napenda burudani Na kujenga urafiki, napenda maisha, napenda familia na nina mapenzi ya kushiriki na binti spesheli. Maisha yanaweza kuwa magumu bila mtu huyo…mimi ni mtu halisi ifikapo masuala ya maisha. Mimi ni mwaminifu, mkarimu, mwenye mapenzi, mcheshi, asiyejali, mtu wa kuaminika, mwenye heshima kwa maisha ya watu wengine…Mimi ni mwanamume anayeishi maisha kama yajavyo. Sijali kuhusu kesho kwa kuwa itakuwepo, haijalishi nifanyacho. Siku bora za baadaye bado zinakuja.*

Kwenye ujumbe huu wa *A1*, mwandishi ajitambulisha kama jemedari mkuu wa majeshi ambayo ni kazi inayopendwa na kutamaniwa na watu kwa ajili ya mshahara wake na staha. Kenrick na wengine (1990) wanadai kuwa wanawake hutafuta na kuangalia wapenzi wa kiume walio na uwezo wa juu wa kijamii na kiuchumi ilhali wanaume hutafuta wapenzi wa kike walio na mvuto mkubwa wa kimaumbile. Wasifu huu wa kibandia utamfanya mlengwa ambaye ni wa jinsia ya kike kuvutiwa. Ili kufikia kiwango cha kuitwa jenerali katika ngazi za kijeshi, lazima uwe umepata masomo ya juu. Vilevile, maelezo yake yanaashiria utajiri mwingi kwa sababu amefanya kazi kwa miongo mitatu. Mwandishi huyu anateka umakinifu wa mlengwa kwa kuonyesha jinsi alivyobobea katika idara ya Uanajeshi kiasi cha kwamba anatumwa katika nchi ya Iraki. Nchi ya Iraki ni mojawapo ya nchi ambazo zinajulikana ulimwenguni kwa sababu ya ukosefu wa usalama hivyo basi wanajeshi hutumwa katika nchi hiyo kila mara ili kupigana na magaidi. Kwa kawaida, mwanajeshi yeyote anayetoka kwao kwenda kudumisha amani hupata hela maradufu. Huu ndio mtego ambao mhalifu huyu anatumia ili kumpata "mpenziwe.''

La kushangaza zaidi ni kuwa anakiri kuwa yu tayari kuacha hata kazi kwa sababu ya mpenzi wake. Anaonyesha kuwa anathamini mapenzi sana kushinda hata kazi yake na kwamba aweza kufanya chochote kile kuyalinda. Mwandishi anadhihirisha mapenzi ya dhati kwa mwandikiwa huku akiahidi kuacha kazi ili kukutana naye. Hii ni njia moja ya kumleta karibu 'mpenzi wake' ili asione ulaghai uliopo bali ayahisi mapenzi ya kweli. Vilevile, mwandishi huyu anajitambulisha kama mtoto yatima na mjane ili iwe njia ya kugusa hisia za mlengwa. Ni wazi kwamba kujitambulisha kama yatima na mjane ni njia moja ya kuonyesha hali ya upweke, upweke utakaomalizwa na mpenzi huyu iwapo atakubali pendekezo lake la kuoana. Ni rahisi kwa mwandishi kutoa ahadi au kusema chochote kile kitakachomfurahisha msomaji kwa sababu yuko mbali na hawaonani.

Ujumbe huu wa kimapenzi unahusisha matumizi ya lugha ya ushawishi pakubwa. Lawson na Leck (2006) wanafafanua kuwa sababu moja ambayo huwafanya au kuwachochea watu kuchumbiana mitandaoni ni kumaliza upweke. Kwenye ujumbe huu, mwandishi ametumia 'picha yake' kwenye mtandao. Katika mtazamo wa kijuujuu na wa haraka wa msomaji, ataweza kuvutiwa na picha hii ili apate kusoma yale yaliyoandamana na picha. Kama alivyodokeza Aristotle katika nadharia ya Ubalagha ya Ushawishi, mkakati wa hisia na kusadika ni njia moja ya kushawishi msomaji au msemaji yeyote yule (Frost. M, 1994). Kuna uwezekano mkubwa kuwa picha ile ni ghushi lakini iliteuliwa kimakusudi ili kumnasa msomaji hasa ikiwa ni wa jinsia ya kike. Mwandishi anatoa maelezo yake ya kibinafsi kuhusu kazi yake, taaluma na hadhi ya ndoa. Anatumia mamlaka kwa kutaja taaluma inayoenziwa na wengi ambayo ni mbinu ya kumnasa msomaji ili apate kuona maisha mazuri aliyonayo mwanajeshi huyu. Maelezo yanayoandamana na picha hasa ya kazi ni baadhi ya mambo ambayo watu hutafuta na kutaka kuyajua wanapotafuta wachumba.

Watafiti wamebaini kuwa wanawake wengi husaka wachumba walio na maisha mazuri na kazi ya kupendeza ilhali wanaume hutafuta wachumba ambao wana mvuto wa sura (Kendrick na wengine, 1990). Mwandishi anatumia mkakati wa hisia kwa kutaja kuwa yeye ni mjane aliyeachiwa mtoto baada

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

ya kifo cha mke wake. Ingawa hajafafanua zaidi kuhusu kisababishi cha kifo cha mke wake, jambo hili linadhihirisha kuwa kwa kweli anahitaji usaidizi. Msomaji atajipata amepatwa na hisia za huruma na hatimaye ataitikia kuwasiliana na mwandishi huyu. Mwandishi amefaulu kwa kutumia mkakati huu wa hisia kwa kutumia mahitaji ya kimsingi ya mwanadamu kwa kuchochea hisia za mapenzi. Anaonyesha hulka zake na namna ambavyo angetaka kuishi na mlengwa. Maelezo yote yaliyotolewa katika ujumbe huu ni kuhakikisha kuwa msomaji amemwamini mwandishi katika hatua za kwanza kabla ya kuendeleza mawasiliano. Mwandishi anahusisha mkakati wa kusadikika na uaminifu. Mkakati huu wa ushawishi huchukua njia mbili zikiwemo: Kujifanya mwenye hulka nzuri kama ilivyo kwenye ujumbe huu na kuonyesha uaminifu kupitia toni pamoja na tajriba kwenye taaluma yake (Baker, M, 2018). Mawasiliano ya Kiupatanishi ya Kitarakilishi kama yalivyofafanuliwa na Herring (2004) kwa kuhusisha mitandao ya kijamii yamesababisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya mwandishi na msomaji.

Buchanan na Whitty (2004) wanaorodhesha hatua saba ambazo hutumiwa na wahalifu wa mitandaoni wanapojaribu kujenga uhusiano wa uchumba. Hatua ya kwanza huwa kutafuta picha nzuri, inayopendeza na yenye mvuto kwa mlengwa halafu picha hiyo hutumiwa kama chambo kwenye ndoano kumvutia mlengwa baada ya kutumiwa ombi la kuwa marafiki. Katika hatua ya pili, wahalifu hujaribu kujenga urafiki kwa kuonyesha uaminifu na kusadikika kwa kuomba namba za simu pamoja na baruapepe. Baada ya hatua hii, wahalifu huzidisha uhusiano kwa kutoa simulizi na vijihadithi vya kibinafsi na kuonyesha hamu ya juu ya kupendezwa na mambo fulani yanayopendwa pia na mlengwa yakiwemo dini na utamaduni. Hatua nyingine huhusisha kubadilishana picha za kibinafsi na jumbe. Hatimaye, mhalifu huomba usaidizi wa hela kiasi kidogo akidai kuwa yuko katika shida fulani kama vile ajali. Wahalifu hawa huendesha uhalifu kwa kuonyesha mamlaka na kuitisha kitita kikubwa cha hela. Cukier na wenzake (2007) wanafafanua mamlaka kama mkakati wa ushawishi unaotumiwa na wahalifu wa mitandaoni wakitafuta wachumba. Wanadokeza kuwa matumizi ya mamlaka husababisha watu kujibu kulingana na amri zinazotolewa na mtu aliye na mamlaka/ cheo cha juu kama inavyodhihirika katika ujumbe huu. Katika ile hali ya kumjibu mwandishi, msomaji hujipata amenaswa katika mtego wa kihalifu bila kutambua.

*Ujumbe A2* wa baruapepe uliandikwa kwa kutumia mtindo wa kiofisi na kwa urasmi mwingi hii ikiwa njia moja ya wahalifu ya kuhakikisha kuwa uhalifu umeonekana kuwa shughuli halali bila mlengwa kugundua.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

**Ujumbe A2**

**From:** Kristalina Georgieva <dfgsxc305@gmail.com>
**To:** "undisclosed-recipients:;" <undisclosed-recipients:;>
**Sent:** Sunday, May 15, 2022, 06:45:13 PM GMT+3
**Subject:** REF: (IMF) KADI YA VISA YA ATM YA UBA / TGR / FGT / 2022.

(I.M.F) OFISI KUU
#1900, AV. DU RAIS
MFUKO WA FEDHA WA KIMATAIFA
KUMB:-XVGNN82022

Mpendwa Mmiliki wa Barua Pepe/Mfaidika wa Mfuko, Nilituma barua hii kwako, mwezi mmoja uliopita, lakini sikusikia kutoka kwako, sina uhakika kama umeipata, Na ndiyo maana nasema tena, Kwanza, mimi ni Bibi Kristalina Georgieva, A. Mkurugenzi Mkuu mpya na Mwenyekiti wa Shirika la Fedha la Kimataifa, tulipata ripoti kwamba hujapokea fedha zako kupitia uhamisho wa benki kama tulivyoagiza awali.
Jina lako lilionekana katika orodha yetu ya ratiba ya malipo ya wanufaika ambao watapokea pesa zao katika malipo haya ya robo ya kwanza ya mwaka kwa sababu tunahamisha fedha mara mbili pekee kwa mwaka kulingana na kanuni zetu za benki. Tunaomba radhi kwa kucheleweshwa kwa malipo yako na tafadhali acha kuwasiliana na ofisi yoyote sasa na uzingatie malipo ya ofisi yetu ipasavyo.

Sasa Malipo yako mapya, Nambari ya Idhini ya Umoja wa Mataifa; UN5685P, Ikulu Iliyoidhinishwa Nambari: WH44CV, Nambari ya Marejeleo-35460021, Nambari ya Mgao: 674632 Nambari ya siri: 339331, Msimbo wa Pini: 55674 na Nambari yako ya Malipo ya Cheti: 103, Nambari Iliyotolewa Nambari: 0763; Uthibitisho wa haraka (IMF) Telex No: -1114433; Nambari ya Siri ya Msimbo: XXTN013. Hazina yako ya urithi wa malipo ya sehemu ni USD $2,500.000.00, baada ya kupokea nambari hizi muhimu za malipo, kwa hivyo umehitimu sasa kupokea na kuthibitisha malipo yako na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Kanda ya Afrika mara moja ndani ya saa 168 zijazo. Tunakuhakikishia kuwa malipo yako yatakufikia mradi tu utafuata maagizo na maagizo yangu. Tumeamua kukupa KASI, KANUNI NI: 601. Tafadhali, wakati wowote unapopokea barua yenye jina Bi. Kristalina Georgieva, angalia kama kuna CODE (601) ikiwa msimbo haujaandikwa, tafadhali futa ujumbe huo. kutoka kwa sanduku lako!

Sisi, Bodi ya Wakurugenzi, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Washington, D.C. kwa kushirikiana na Idara ya Hazina ya Marekani na Mashirika mengine husika ya Uchunguzi hapa Marekani. Ameagiza Kitengo chetu cha Utumaji Pesa za Malipo ya Kigeni, United Bank of Africa Lome Togo kukupa Kadi ya VISA, ambapo hazina yako ya $2,500,000.00 itapakiwa, kwa uondoaji zaidi wa hazina yako.
Wakati wa uchunguzi wetu, tuligundua kwa masikitiko kwamba malipo yako yamecheleweshwa isivyofaa na maafisa wafisadi wa Benki ambao wanajaribu kuelekeza fedha zako kwenye akaunti zao za kibinafsi.

Unashauriwa KUTOPELEKA malipo zaidi kwa taasisi yoyote kuhusiana na muamala wako kwani hazina yako itatumwa kwako moja kwa moja kutoka kwa chanzo chetu.
Na leo tunakujulisha kwamba mfuko wako umeingizwa kwenye Kadi ya VISA na Benki ya UBA na pia tayari kutumwa. Sasa wasiliana na Huduma kwa Wateja wa Benki ya UBA.
MR.KENNEDY UZOKA
Barua pepe: infor.atmoffice@gmail.com
Mtumie taarifa ifuatayo kwa ajili ya kuletewa Kadi yako ya VISA ya ATM iliyoidhinishwa kwa anwani yako ya nyumbani.

Kuwa mkarimu na uwasiliane na United Bank of Africa kupitia barua pepe hii hapa chini:

(https://www.pcrisk.com/removal-guides/20241-international-monetary-fund-imf-email-scam).

Ujumbe A2 unadhihirisha urasmi kwa kuhusisha jina na mwandishi na baruapepe yake, anwani, tarehe, saa, siku, mada na marejeleo. Itakuwa vigumu sana kwa msomaji au mlengwa kuushuku ujumbe. Utumiaji wa urasmi ni njia moja ya kuhakikisha kuwa mwandishi amesadikika katika hatua ya kwanza. Kutomnasa msomaji katika hatua ya kwanza ni kumpoteza na pia kupoteza bahati yake ya kutekeleza uhalifu. Mwandishi huyu anadhihirisha upole kwa kumrejelea mwandikiwa kama mpendwa kisha anafululiza kusema kuwa yeye ni Mkurugenzi mpya wa Shirika la Kimataifa. Sehemu hii ni muhimu katika kumshawishi mwandikiwa kwa mwandishi kudhihirisha kuwa ni mtu aliye na mamlaka ya Kimataifa. Dyrud (2005) anasema kuwa wahalifu hutumia mamlaka kujifananisha na watu wakubwa katika mashirika au wakurugenzi kwenye benki na hujaribu kuelezea kuhusu uhalali wa pesa kama njia ya kuwashawishi walengwa.

'Mkurugenzi' huyu anaelezea mwandikiwa kuwa yeye ni miongoni mwa wale ambao watapata malipo kama ilivyo desturi ya shirika lile. Kutaja uhamisho wa pesa ni kichocheo kwa mwandikiwa ambacho hawezi akakipuuza kamwe. Kadhalika, mwandishi anaelezea kuwa huwa wanafanya uhamisho mara mbili kwa mwaka. Sehemu hii itamfanya mwandikiwa kuwa makini kwa sababu inaonekana kuwa ikiwa hatapata zile pesa inawezekana azipate mwaka ujao. Mwandishi ametumia mkakati wa mantiki ili kuhakikisha kuwa mwandikiwa atawasiliana na 'mkurugenzi' kuhusiana na fedha hizo. Mwandikiwa anaomba msamaha kwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mwandikiwa kwa ajili ya kucheleweshwa kwa pesa zake. Matumizi ya kiimbo cha upole na unyenyekevu ni mbinu za kuonyesha uaminifu na kumfanya mlengwa kuamini. Naksawat na wenzake (2016) anasema kuwa wahalifu hujifanya wapole na wanyenyekevu katika mazungumzo ili kujenga uhusiano mzuri na walengwa. Mwandishi anamtahadharisha mlengwa kuwa awache kuwasiliana na ofisi yoyote isipokuwa wao. Hali hii itamfanya mlengwa kutofahamisha watu wengine watakaomzindua kuhusu uhalifu huu hivyo mhalifu kufaulu kutumia mantiki ili kuhakikisha kuwa mlengwa ameshirikiana naye hadi wakati ambapo uhalifu utapotekelezwa. Mwandishi pia anatoa maelezo mengi yatakayomsaidia mlengwa kupokea fedha kama vile nambari ya siri, marejeleo, nambari ya mgao na anwani. Mwandishi ametumia mkakati wa uaminifu na kusadikika ili kuhakikisha kuwa hajampoteza mlengwa.

Matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ya kwanza wingi ni muhimu ili kuondoa ubinafsishaji wa shughuli hizi na angetaka mazungumzo yote yaonekane kuwa yamehusisha watu wengi hivyo kujenga uhalali na kuweka ujumbe uzito. Anaelezwa kuwa, ‘tunakuhakikishia kuwa utapokea malipo ikiwa utafuata maagizo’. Bernard na Hunter (2008) wanafafanua kuwa taasisi huhusisha mawakala wengi wanaofanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya lengo moja. Maagizo na hatua za kufuata zinazotolewa kwenye ujumbe ni mbinu ya kumshawishi mlengwa atoe maelezo yake ya kibinafsi ambayo ni hatua muhimu sana kwa mwandishi kwa sababu ataweza kutekeleza uhalifu baada ya kupata habari za kimsingi zinazomhusu mlengwa. Atkins na Huang (2013) wanafafanua kuwa wahalifu huwachangamsha wasomaji kwa kuwafanya wahisi kuwa wameaminiwa na kuteuliwa kushiriki katika shughuli fulani kama ilivyo katika ujumbe huu.

Zaidi ni kuwa, ujumbe huu umerudia sababu zilizomfanya mwandikiwa kucheleweshewa pesa zake hata ingawa haya yalikuwa yamefafanuliwa awali. Hii ni mbinu ya kutilia mkazo ili suala hili lionekane kuwa na uzito. Hata hivyo, kwenye hatua hii mwandishi ametoa sababu nyingine ya maafisa wafisadi kuwepo katika shirika na kumwonya asipeleke malipo kwa taasisi nyingine. Hii ni njia ya kuonyesha uaminifu kwa kuonekana kuwa wanakashifu ufisadi. Utumiaji wa herufi kubwa kwenye neno ‘kutopeleka’ ni kumsisitizia mlengwa kutohadaiwa tena. Ujumbe huu ni wa kihalifu na umetumia mkakati wa uaminifu kumshawishi mwandikiwa. Usimulizi huu mrefu ni muhimu kwa sababu umetoa maelezo kwa kina yatakayomfanya mwandikiwa kuamini kuwa ni ya kweli. Chau na wenzake (2002) anasema kuwa jumbe ndefu hushawishi zaidi kushinda jumbe fupi katika mawasiliano sawa na ilivyo katika ujumbe huu.

*Ujumbe wa A3* unadhihirisha utapeli wa kibiashara unaofanyika kwa njia ya masimulizi marefu ili kuhakisha kuwa mhalifu amefafanua kwa kina yatakayomgusa mlengwa.

**Ujumbe A3**

| | |
|---|---|
| ***Subject:*** | *Hello My Dear,* |
| ***Date:*** | *Sat, 2 Feb 2013 12:08:49 +0000* |
| ***From:*** | *SamiraKipkalya <samira.kipkalya@sify.com>* |
| ***Reply-to*** | *< samira.kipkalya@sify.com>* |
| ***To:*** | *undisclosed recipients:;* |

*Hello My Dear, PLEASE I NEED YOUR HELP*

*My Name is Samira I am writing this mail to you with tears and sorrow from my heart. With due respect, trust and humanity, i appeal to you to exercise a little patience and read through my letter, I wish to contact you personally for a long term business relationship and investment assistance in your Country so i feel quite safe dealing with you in this important business having gone through your remarkable*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*profile, honestly i am writing this email to you with pains, tears and sorrow from my heart, i will really like to have a good relationship with you and i have a special reason why i decided to contact you, i decided to contact you due to the urgency of my situation, reason why i decided to contact you, My name is Miss. Samira Kipkalya Kones, 23yrs old female and I held from Kenya in East Africa. My father was the former Kenyan road Minister. He and Assistant Minister of Home Affairs Lorna Laboso had been on board the Cessna 210, which was headed to Kericho and crashed in a remote area called Kajong'a, in western Kenya. The plane crashed on the Tuesday 10th, June, 2008. You can read more about the crash through the below site: http://edition.cnn.com/2008/WORLD/africa/06/10/kenya.crash/index.html*

*After the burial of my father, my stepmother and uncle conspired and sold my father's property to an Italian Expert rate which the shared the money among themselves and live nothing for me. I am constrained to contact you because of the abuse I am receiving from my wicked stepmother and uncle. They planned to take away all my late father's treasury and properties from me since the unexpected death of my beloved Father. Meanwhile i wanted to escape to the USA but they hide away my international passport and other valuable travelling documents. Luckily, they did not discover where i kept my fathers File which contains important documents. So I decided to run to the refugee camp where i am presently seeking asylum under the United Nations High Commission for the Refugee here in Ouagadougou, Republic of Burkina Faso.*

*One faithful morning, I opened my father's briefcase and found out the documents which he has deposited huge amount of money in bank in Burkina Faso with my name as the next of kin. I travelled to Burkina Faso to withdraw the money for a better life so that I can take care of myself and start a new life, on my arrival, the Bank Director whom I met in person told me that my father's instruction/will to the bank is that the money would only be release to me when I am married or present a trustee who will help me and invest the money overseas. I am in search of an honest and reliable person who will help me and stand as my trustee so that I will present him to the Bank for transfer of the money to his bank account overseas. I have chosen to contact you after my prayers and I believe that you will not betray my trust. But rather take me as your own sister.*

*Although, you may wonder why I am so soon revealing myself to you without knowing you, well I will say that my mind convince Ed me that you may be the true person to help me. More so, my father of blessed memory deposited the sum of (US$11.500, 000) Dollars in Bank with my name as the next of kin. However, I shall forward you with the necessary documents on confirmation of your acceptance to assist me for the transfer and statement of the fund in your country. As you will help me in an investment, and i will like to complete my studies, as i was in my 1year in the university when my beloved father died. It is my intention to compensate you with 30% of the total money for your services and the balance shall be my capital in your establishment. As soon as I receive your positive response showing your interest I will put things into action immediately. In the light of the above. I shall appreciate an urgent message indicating your ability and willingness to handle this transaction sincerely.*

*AWAITING YOUR URGENT AND POSITIVE RESPONSE, Please do keep this only to your self for now un till the bank will transfer the fund. I beg you not to disclose it till i come over because I am afraid of my wicked stepmother who has threatened to kill me and have the money alone ,I thank God Today that am out from my country (KENYA) but now In (Burkina Faso) where my father deposited the money with my name as the next of Kin.*

*I have the documents for the claim.*

*Yours Sincerely Miss.*

*Samira Kipkalya Kones.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*Habari mpenzi wangu, tafadhali nahitaji msaada wako. Jina langu ni Samira na ninakuandikia ujumbe huu nikiwa na machozi na huzuni nyingi moyoni. Kwa heshima inayostahili, uaminifu na ubinadamu, naomba uwe na subira kidogo usome barua hii yangu. Ningependa kuwasiliana nawe kuhusu uhusiano wa muda mrefu wa kibiashara na usaidizi wa uwekezaji katika nchi yako. Nahisi ni salama kabisa kuhusiana na wewe katika biashara hii muhimu baada ya kupitia maelezo yako na wasifu. Kwa uaminifu, ninakuandikia baruapepe hii nina uchungu, machozi na majonzi kutoka moyoni na ninependa sana kuwa na uhusiano mzuri nawe na ndio sababu yangu kuwasiliana nawe. Nimeamua kuwasiliana nawe kwa sababu ya udharura wa suala hili langu. Jina langu ni Bi. Samira Kones, mwanamke wa miaka 23 kutoka nchi ya Kenya iliyo Africa Mashariki. Babangu alikuwa waziri wa kitambo wa barabara. Yeye pamoja na waziri wa masuala ya ndani ya nchi kwa jina Lorna Laboso walikuwa wameabiri ndege iliyoanguka ikielekea Kericho katika sehemu iitwayo Kajong'a katika Magharibi mwa nchi ya Kenya. Unaweza kusoma mengi kuhusu ajali hiyo kwenye tovuti ifuatayo: http://edition.cnn.com/2008/WORLD/africa/06/10/kenya.crash/index.html*

*Baada ya mazishi ya babangu, mamangu wa kambo na mjomba walipanga njama ya kuuuza mali za babangu kwa Mwiitaliano na wakagawana pesa bila kuniachia chochote. Nimelazimika kuwasiliana nawe kwa ajili dhuluma ninakopata kutoka kwa mama wa kambo na mjomba. Walipanga kuchukua hazina yote ya babangu pamoja na mali baada ya kifo kisichotarajiwa cha babangu mpendwa. Nilitaka kutorokea Marekani lakini wakaficha pasipoti yangu ya kimataifa na nakala nyinginezo za usafiri. Kwa bahati nzuri, hawakufaulu kupata nilikokuwa nimeficha faili za babangu zilizokuwa na nakala muhimu. Niliamua kukumbia katika kambi za ukimbizi ambapo nimepata kimbilio nikisaidiwa na shirikika la UN katika nchi ya Burkina Faso. Asubuhi moja nzuri nilifungua mkoba wa babangu na kupata stakabadhi kuwa alikuwa amehifadhi pesa nyingi sana katika benki ya Burkina Faso na jina langu kama jamaa wa kufaidika.*

*Nilisafiri katika nchi ya Burkina Faso ili nitoe pesa kwenye benki ili maisha yangu ya baadaye yawe mazuri lakini Mkurugenzi mkuu kwenye benki alinifahamisha kuwa nitapata pesa zile ikiwa nitakuwa nimeolewa au nionyeshe mdhamini ambaye atanisaidia kuwekeza pesa hizi katika nchi za nje. Ninamtafuta mtu mwaminifu na wa kusadikika atakayekuwa mdhamini wangu ili niwasilishe jina lake kwenye benki. Nimeamua kuwasiliana nawe baada ya maombi na naamini kuwa hutanisaliti na utanichua kama dadako. Ingawa unaweza kuwa unawaza sababu yangu kujitambusha kwako bila kukujua, naweza kusema kuwa mawazo yangu yamenibainishia kuwa unaweza kuwa mtu mzuri wa kunisaidia.*

*Zaidi ya haya, babangu alihifadhi dola 11.500,000 kwenye benki zikiwa na jina langu. Nitakutumia nakala zangu muhimu ili uthibitishe usaidizi wako kwangu na stakabadhi za kuhamisha pesa katika nchi yako. Utakaponisaidia katika uwekezaji nitataka pia kukamilisha masomo yangu kwa kuwa nilikuwa mwaka wa kwanza katika chuo kikuu wakati babangu mpendwa aliaga dunia. Nitakuzawidi kwa asilimia 30 % ya pesa hizo kwa ajili ya usaidizi na masalio yatakuwa yangu ya kuanza biashara. Punde tu nitakapopata ujumbe wako nitashughulika mara moja. Kuhusiana na suala hizi, nitashukuru kwa ujumbe wako mara moja wa kuonyesha uwezo na ari ya kushughulikia fedha hizi kwa uaminifu. Ninasubiri majibu yako kwa dharura na nakusihi uweka kama siri hadi wakati ambapo benki itahamisha pesa hizo. Nakusihi usimfahamishe mtu yeyote kuhusu haya kwa sababu ni hofu kuhusu mama yangu wakambo ambaye ni mwovu na ametishia kuniua na achukue pesa hizi peke yake. Namshukuru Mungu leo kwa kuweza kutoka katika nchi yangu Kenya na kwa sasa niko Burkina Faso ambapo babangu alihifadhi pesa na akatumia jina langu kama jamaa wa kusaidika. Nina stakabadhi za kufanya madai*

*Samira Kipkalya Kones (https://nairobipublicsquare.wordpress.com/2011/08/14/46/).*

Mwandishi ametumia mbinu rejeshi pakubwa kuelezea yaliyotokea kwenye *ujumbe A3*. Anaelezea kuwa wakati baba yake alipokuwa kiongozi aliweza kuhamisha pesa nyingi katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

akaunti yake. Sehemu hii ya kutaja fedha katika hatua ya kwanza ni kichocheo kinachokusudiwa kugusa hisia za msomaji ili washirikiane kwa kuusoma ujumbe huu kikamilifu hadi mwisho. Mwandishi anaeleza mwaka ambao baba yake alipokuwa katika utawala ikiwa ni njia moja ya kuonesha ukweli wa ujumbe wenyewe. Kadhalika, mwandishi anajinasibisha na kiongozi katika nchi kama njia moja ya kumshawishi msomaji asije akamwona kama mtu wa kawaida. Hali hii ya kujishaua ni jambo la kawaida katika simulizi kama hizi kwa sababu madhumuni makuu ya wahalifu ni kuwalaghai watumiaji wa baruapepe kwa kujifanya walivyo watu tajika ili kuuficha uovu wao. Uzito zaidi katika sehemu hii unajitokeza wakati ambapo mwandishi anasema kuwa stakabadhi zote za uhifadhi zipo kama njia ya kuonyesha uhalali na ukweli wa kile kinachozungumziwa ikiwa ni njia ya ushawishi. Mwandishi anatumia tukio la kisiasa lililosababisha kifo cha baba yake mpendwa, tukio halisi ambalo limewahi kushuhudiwa katika nchi nyingi za Afrika. Itakuwa rahisi kuamini yale yanayosimuliwa kwa sababu ni matukio ya kikawaida katika bara hili.

Mwandishi anaweka uzito wa ujumbe wake kwa kuibua tukio la kusikitisha kuhusu kifo cha babake kilichotokana na kivangaito cha kisiasa. Ametumia mkakati wa hisia ili kugusa hisia za msomaji kwa kutaka kuhurumiwa kutokana na kumpoteza mzazi wa kiume. Amehusisha pia mkakati wa mantiki wa ushawishi kwa kufafanua sababu ya pesa zile kuhifadhiwa katika nchi ya kigeni. Hali hii ilichangiwa sana na machafuko yaliyoshuhudiwa katika nchi yao. Kwa msomaji yeyote atakayeguswa na kijihadithi hiki atajipata ameingia kwenye mtego huu wa mhalifu. Mwandishi anafululiza kushawishi zaidi anaposema kuwa wameamua kuwasiliana na mlengwa ili awafae katika shughuli hizi za uhamishaji pesa. Sehemu hii ni muhimu kwa msomaji aliye makini kung'amua kuwa ujumbe huu ni wa kilaghai kwa sababu katika hatua ya mwanzo, mwandishi alieleza kadhia hii akiwa pweke. Hata hivyo, nafsi imebadilika na kutumia kiwakilishi cha nafsi wingi kuashiria kuwa ujumbe unahusisha watu wengi hali ambayo ni tatanishi kueleweka.

Anatumia ushawishi zaidi kwa kumpa mlengwa nafasi katika shughuli hizi anapodai kuwa tunaomba usaidizi wako katika uhamishaji wa fedha hizi. Kumpa mwandikiwa nafasi ni ushawishi unaonuiwa kumwonyesha kuwa atafaidika mno ikiwa atashirikiana na mwandishi. Anazidisha utumiaji wa mkakati wa hisia kwa kujenga taswira ya hali ilivyokuwa katika nchi yao wakati tandabelua hii ilipotokea. Anazungumzia kuhusu kuharibiwa kwa majengo, mali kuibiwa na cha kuhuzunisha zaidi ni kupoteza jamaa zake wakiwemo baba, ndugu ya babake na mama yake. Anaonyesha upweke alionao katika nchi ya kigeni na angali mkembe. Hii inatagusa hisia za mwandikiwa ili aweze kumhurumia. Hatua ya mwisho inaelezea jinsi mama yake mwandishi alivyomfahamisha kuhusu pesa na umuhimu wa kuomba ili apate mtu mwaminifu atakayemfaa kuwekeza. Mwandishi anajisawiri kama mtu mcha Mungu kwa kuonyesha umuhimu wa kufanya maombi kabla ya kushughulikia jambo hili adhimu. Watu waumini ni rahisi kuaminiwa kushinda wasio waumini hivyo mwandishi amejifungamanisha na suala la imani kama njia ya kumshawishi mlengwa. Ikiwa mlengwa ni mtu wa imani kama mwandishi, itakuwa rahisi kwake kumnasa na kutekeleza uhalifu wake.

Ujumbe A4 ni mfano mzuri wa ujumbe wa kihalifu unaoonyesha jinsi wahalifu hudai kuwa wanatoa usaidizi kwa walio na mahitaji kwenye Facebook ila nia yao huwa kutekeleza uhalifu.

**Ujumbe A4**

*Please, I beg you in the name of God to help me collect the $15Million and interest accrued on the deposit from Allied Bank and distributes it amongst charity organizations. You are at liberty to use your discretion to distribute the money and feel free as well to reimburse yourself when you have the money for any*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*expenses you incur in the course of collecting and distributing the money to charity organization. I am willing to reward you for your assistance and kindness.*
*Tafadhali nakuomba katika jina la Mungu unisaidie kuchukua $15 milioni Na riba ya uwekezaji kutoka kwenye Allied Bank na usambazie mashirika ya misaada. Una uhuru wa kutumia busara yako kusambaza pesa hizi na uwe kujifidia ikiwa una mahitaji yoyote katika shughuli za kuchukua na kusambaza pesa hizi za misaada. Niko tayari kukuzawidi kwa usaidizi na ukarimu wako (Police Scotland Edinburgh FRAUD DOING THE ROUNDS-FACEBOOK).*

Katika ujumbe wa A4 kuna ombi kutoka kwa mwandishi kwa msomaji wa ujumbe akimtaka amsaidie kusambaza pesa nyingi kwa watu pamoja na riba kwa mashirika ya misaada. Mwandishi huyu ni tajiri kama anavyojisawiri. Anafanya ombi lake kwa kutumia maneno ya heshima kama "tafadhali" na kuhusisha jina la Mwenyezi Mungu. Anamweleza msomaji ambaye ndiye mpokeaji wa pesa kuwa ana uhuru wa kutumia pesa hizi wakati anaposhughulikia usambazaji huu. Baada ya shughuli za kusambaza, mwandishi anamwahidi msomaji/mpokeaji kuwa angemzawidi kwa ajili ya usaidizi wake. Mazungumzo haya yana mvuto zaidi kwenye macho ya msomaji na kwa namna ambavyo mwandishi anavyodhihirisha unyenyekevu na upole. Inashangaza jinsi ambavyo mtu anaweza kumwaminia mtu asiyemfahamu dola milioni kumi na tano na anafaa atekeleze anachoambiwa kwa mazungumzo ya baruapepe. Kutaja mamilioni ya pesa pamoja na lugha ya rai ni kivutio kwa msomaji wa ujumbe ili aweze kuamini kila kitu anachoambiwa na akitekeleze pasi kufikiria mengi. Msomaji anafaa agutuke kwa sababu ahadi ambazo zimetolewa haziwezi kuwa za kweli. Kauli yenye mantiki na inayoashiria ukweli imetumiwa na mwandishi anapomwomba mlengwa kumsaidia kusambaza pesa kwa watu wahitaji.

Mkakati wa imani wa ushawishi umetumiwa pia na mwandishi kwa kujifanya kuwa yeye ni Mcha Mungu ili chochote anachokizungumzia kichukuliwe kuwa ni cha ukweli. Mlengwa atashawishika upesi hasa ikiwa yeye ni muumini. Kutaja pesa nyingi namna hii ni njia moja ya kugusa hisia za msomaji. Kwa uhakika, mwandishi anajisawiri kama mtu mwenye utu, msaidizi na mnyenyekevu. Uteuzi wake wa maneno pamoja na kiimbo ni ushawishi mkubwa kwa msomaji na itakuwa rahisi kwake kunaswa na mtego wa mwandishi.

## HITIMISHO

Utafiti huu ulilenga vipengele muhimu vya ushawishi vinavyodhihirika katika jumbe za kimasimulizi za wahalifu kwenye mitandao ya kijamii. Jumbe hizi za kihalifu zilionekana kusheheni sifa zinazofanana za kiushawishi pamoja na mbinu sawa za lugha. Mbinu za lugha zinazojitokeza katika jumbe hizi ni kama vile, takriri, mdokezo, herufi kubwa, herufi nzito, nidaa, chuku, mbinu rejeshi, taswira na nyinginezo. Ingawa ni muhali kumaliza uhalifu huu kwenye mitandao ya kijamii, ni muhimu kuelewa baadhi ya mikakati ya ushawishi pamoja na mbinu za lugha zinazotumiwa mno na wahalifu hawa kuwashawishi watu. Mikakati ya ushawishi iliyojitokeza kwenye utafiti huu ni: Mkakati wa hisia, mkakati wa mantiki na mkakati wa imani na maadili. Wahalifu walitumia mkakati wa hisia ili kunasa hisia za msomaji na walitumia zaidi simulizi ndefu zenye mvuto, urudiaji wa kauli fulani pamoja na matumizi ya herufi kubwa. Mkakati wa imani ulitumiwa pakubwa katika jumbe hizi kwa kutaja jina la Mwenyezi Mungu na wahalifu kujifanya wacha Mungu ili kudhihirisha sifa za unyenyekevu, upole na uaminifu. Mkakati huu wa ushawishi ni mbinu moja ya kugusa akili ya msomaji kwa kujificha katika imani na dini na bila shaka mtu yeyote ambaye ni mfuata dini atakubaliana na maombi ya mwandishi.

Mkakati wa hisia ulitumiwa pia na wahalifu kwa kuibua tukio la kusikitisha kama vile kifo cha mpendwa, vita na athari zake, upweke na mengine mengi. Wahalifu walitumia kauli ambazo zina uzito

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

zinazogusa hisia za wasomaji ili waweze kuhurumiwa. Katika kitendo cha kumhurumia mwandishi, msomaji tayari alikuwa ameanguka kwenye mtego wa kihalifu. Vilevile, ilibainika kuwa jumbe hizi za kihalifu husheheni utumiaji wa mkakati wa mantiki kwa wingi. Wahalifu walitoa hoja zenye mantiki ili jumbe zao ziweze kuaminika. Wahalifu kujifanya waaminifu na wakweli ni mbinu inayowafanya wasomaji wa jumbe hizi kukubaliana na chochote kilichopendekezwa na wahalifu hawa. Chiluwa (2015) anasema kuwa changamoto za kiuchumi za kidunia zinaweza kuchangia kuongezeka kwa uhalifu wa mitandaoni na visa vya udanganyifu kwenye intaneti.

## MAREJELEO


Atkins, B., & Huang, W. (2013). A study of social engineering in online frauds. *Open Journal of Social Sciences, 1(03)*, 23.

Baker, M. (2018). *Structured writing: rhetoric and process*. XML Press, 2018.

Buchanan, T., & Whitty, M. T. (2014). The online dating romance scam: causes and consequences of victimhood. *Psychology, Crime & Law*, *20*(3), 261-283.

Chau, P. Y., Cole, M., Massey, A. P., Montoya-Weiss, M., & O'Keefe, R. M. (2002). Cultural differences in the online behavior of consumers. *Communications of the ACM*, *45(10)*, 138-143.

Chiluwa, I. (2015). *Email fraud. International encyclopedia of language and social interaction*. Malden: Masachussetts: Wiley-Blackwell.

Crystal, D. (2011). *Internet linguistics: A student guide*. Routledge.

Cukier, W. L., Nesselroth, E. J., & Cody, S. (2007, January). Genre, narrative and the" Nigerian Letter" in electronic mail. In *2007 40th Annual Hawaii International Conference on System Sciences (HICSS'07)* (pp. 70-70). IEEE.

Dyrud, M. A. (2005, October). I brought you a good news: An analysis of Nigerian 419 letters. In *Proceedings of the 2005 Association for Business Communication Annual Convention* (pp. 20-25).

Fadhilah, N. U. (2010). A Discourse analysis on the persuasive techniques used in DRTV advertisement. *Unpublished Thesis. Malang UIN Maulana Malik Ibrahim Malang.*

Frost, M. (1994). Ethos, Pathos & (and) Legal Audience. *Dick. L. Rev*.,99,85.

Hayward, K., & Yar, M. (2006). The ‘chav’phenomenon: Consumption, media and the construction of a new underclass. *Crime, media, culture*, 2(1), 9-28.

Lawson, H. M., & Leck, K. (2006). Dynamics of internet dating. *Social Science Computer Review*, *24*(2), 189-208.

Lea, S. E., Fischer, P., & Evans, K. M. (2009). The psychology of scams: Provoking and committing errors of judgement.

Kenrick, D. T., Sadalla, E. K., Groth, G., & Trost, M. R. (1990). Evolution, traits, and the stages of human courtship: Qualifying the parental investment model. *Journal of personality*, *58*(1), 97-116.

Ling, R., & Baron, N. S. (2007). Text messaging and IM: Linguistic comparison of American college data. *Journal of language and social psychology*, 26(3), 291-298.

Mann, D., & Sutton, M. (1998). >> NETCRIME: more change in the organization of thieving. *The British Journal of Criminology*, *38*(2), 201-229.

Modic, D., & Lea, S. E. (2013). Scam compliance and the psychology of persuasion. *Available at SSRN 2364464*.

Montague, S. (2011). Genetic suspects: global governance of Forensic DNA profiling and Databasing. *The Yale Journal of Biology and Medicine*, *84*(3), 326.

Nabea, W. (n.d)Persuasive Strategies employed by Cyber Criminals: The Case of the Fraud-Email Narrative. *Contemporary Social Sciences*, 85.

Naksawat, C., Akkakoson, S., & Loi, C. K. (2016). Persuasion strategies: use of negative forces in scam e-mails. *GEMA Online® Journal of Language Studies*, *16*(1), 1-17.

Perloff, R. M. (2013). Political persuasion. *The SAGE handbook of persuasion: Developments in*


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1227

*theory and practice*, 258-77.

Rusch, J. J. (1999, June). The "social engineering" of internet fraud. In *Internet Society Annual Conference, http://www. isoc. org/isoc/conferences/inet/99/proceedings/3g/3g _2. htm*.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.